HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MJI MPYA
S.L.P. 8480 – MOSHI KILIMANJARO.

Kumb.Na.MMSS/S.2026/ADM.F.I/2020 TAREHE 16/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI……

1.0: YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MJI MPYA MANISPAA YA MOSHI MWAKA – 2021

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa na Taifa kujiunga Kidato cha kwanza katika shule ya sekondari MjiMpya. Nakukaribisha sana na ni matumaini yangu kuwa utapokea nafasi uliyopewa na Taifa kwa kutimiza wajibu wa kujifunza na kufanya kazi kwa bidii. Ni nafasi ya pekee kwako.

Mara upatapo fomu hii zingatia maelekezo uliyopewa ili uweze kupokelewa shuleni. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021 saa 1.30 asubuhi** kwa ajili ya usajili. Mzazi/mlezi afike shuleni tarehe **04/01/2021 saa nne asubuhi** kwa ajili ya kikao cha wazazi wa wanafunzi wote wa kidato cha kwanza **2021. Kwenye kikao hicho mtakutana pia na kamati ya chakula ya wazazi.Gharama ya chakula ni Tshs 70,000/= kwa mwaka. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Namba 40303100002 Benki ya NMB. Unaweza kulipa fedha yote au nusu yake na kumalizia iliyobaki muhula wa pili.Wasilisha risiti ya kulipia fedha hizo shuleni(Bank pay in slip Original). NI WAJIBU W A KILA MZAZI/MLEZI KUMLIPIA MWANAE FEDHA YA CHAKULA CHA MCHANA SHULENI. WAZAZI/WALEZI MNAKARIBISHWA SANA KWENYE KIKAO.**

Masomo yanayofundishwa hapa shuleni ni **Uraia, Kiswahili, Kiingereza, Hisabati, Historia, Jiografia, Baologia, Fizikia, Kemia na masomo ya Biashara.**

2.0: SARE YA SHULE:

2.1: WAVULANA.

- Suruali 2 - Rangi ya **"NYEUSI".** Suruali chini isipungue mzunguko wa **Inchi 16. (INASISITIZWA. IKIWA CHINI YA HAPO HATAPOKELEWA AU ITAKATIWA KWENYE GOTI)**
-Mkanda mweusi
- Shati 2 - Nyeupe mikono mifupi
- Sweta 1 - Rangi ya **"KIJANI" SHINGO YA "V"**

-Nembo mbili za shule **(NI MUHIMU SANA) Hii hupatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 1,000/= kwa kila moja.**
-Soksi nyeupe

2.2: WASICHANA.

Edit with WPS Office

- Sketi 2 - Rangi ya **"NYEUSI"**
- Blauzi/shati 2 - Nyeupe mikono mifupi
- Sweta 1 - Rangi ya **"KIJANI" SHINGO YA "V"**

Mshono wa sketi uwe **"RINDA BOX" Na iwe ndefu mpaka kwenye kisigino.**

-Nembo mbili za shule **(NI MUHIMU SANA)Hizi hupatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 1000/= kwa kila moja.**

2.3: <u>WASICHANA WAISLAMU (WANAOVAA MAVAZI YA KIISLAMU):</u>

- Shungi 2 nyeupe - Zisiwe na Urembo wowote.
- Panjabe 2 nyeupe
- Sweta - 1 – Rangi ya **" KIJANI " SHINGO YA "V"**

Mshono wa Sketi ni Rinda Box na iwe ndefu mpaka kwenye kisigino.

-Soksi nyeupe **(Zisiwe na urembo wowote)**

-Nembo 2 za shule **(NI MUHIMU SANA) Hizi hupatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 1000/= kwa kila moja.**

3.0: <u>KWA WANAFUNZI WOTE</u>.

(i) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba, visiwe na kisigino kirefu na pia visiwe na mapambo.**(VIATU MAARUFU KWA JINA BAJAJI HAVIRUHUSIWI KABISA)**

(ii) Soksi za rangi nyeupe – **zisiwe na mapambo wala maandishi.**

4.0: MAHITAJI YA MASOMO.

(i) Begi la shule lisilo na mapambo wala maandishi.
(ii) Madaftari makubwa 13 **(counter books).**
(iii) Kalamu za wino na risasi.
(iv) Mathematical set moja.
(v) Kamusi ya kiingereza (Oxford Student's Dictionary) hii ni mali binafsi ya mwanafunzi na ni muhimu mwanafunzi kuwa nayo kwani masomo ya sekondari hufundishwa kwa lugha ya kiingereza.
vi) Kila mwanafunzi aje na REAM A4 kwa ajili ya mazoezi na mitihani.
vii) Kila mwanafunzi aje na picha moja(passport size) na file moja la kaki

TANBIHI: Shule haina uwezo wa kuwapa wanafunzi wote vitabu vya kutosha vya rejea hivyo unapaswa kujinunulia vitabu kila utakapoona pana upungufu.

Edit with WPS Office

MAHUDHURIO:

1. Wanafunzi wanatakiwa kuwepo shuleni muda wote wa saa za shule.
2. Wanafunzi wanatakiwa kuwahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama usafi wa mazingira, shughuli za uzalishaji mali, michezo . Atakaye chelewa au kukosa ataadhibiwa.
3. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbia mahali atakiwapo asikiapo kengele au mwito mwingine wowote.
4. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni katika tarehe zilizopangwa mwanzoni mwa kila muhula au baada ya mapumziko ya aina yoyote.

ANGALIZO

Ruhusa ya kutokuwa shuleni siku moja au zaidi ni lazima itoke kwa Mkuu wa shule au Makamu Mkuu wake. Mzazi /Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye atakayehusika kumwombea mwanafunzi ruhusa na siyo mtu mwingine.

MIPAKA YA SHULE:

Mipaka ya shule ni eneo lote la shule kama litakavyotambulishwa na shule. Wakati wote wa masomo wanafunzi watatakiwa kuwa eneo la shule la sivyo watahitaji vibali maalumu kuwa nje ya mipaka hiyo.

UTARATIBU WA MASOMO: Siku za masomo ni kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa. Mwanafunzi afike kila siku **asubuhi saa 1.00** Kamili kwa **"roll call"** usafi na matangazo muhimu. Masomo ya darasani yanaanza **saa 1.30 asubuhi**. Ni lazima mwanafunzi awahi ili kushiriki shughuli za nje na hatimaye kipindi cha kwanza cha masomo.

USAFI:

1. Usafi wa mtu binafsi.

Ni lazima mwanafunzi awe msafi na nadhifu, anyoe nywele ziwe fupi. Kufuga ndevu ni marufuku, kucha ziwe fupi bila rangi. Nguo ziwe zimenyooka, viatu viwe na hali nzuri na vipakwe rangi.

2. a) Usafi wa mazingira. Ni wajibu kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali ya usafi wakati wote. Uchafu na takataka ni lazima zitupwe mahali panapostahili.**(Shimo la taka).**

b)Kwa kuzingatia swala la usafi:

i) Kila mvulana aje na ufagio mmoja mkubwa na " **squizer"**

ii) Kila msichana aje mfagio wa chelewa, na **"hard broom"**

Vifaa hivi vitapokelewa shuleni siku mwanafunzi anaporipoti/sajiliwa. Mwanafunzi atatumia vifaa hivi kufanya usafi kwenye eneo lake mwenyewe.

3. TABIA NA MWENENDO

(a) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvuta tumbaku ya aina yoyote, kutumia kilevi cha aina yoyote, kuvuta bangi, kulewa, kuiba na kutumia lugha chafu.

(b) Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda kwenye majumba ya starehe. Pia kwenye

Edit with WPS Office

nyumba za watumishi wa shule

(c) Nimarufuku mwanafunzi kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi ndani nan je ya sghule..

UMUHIMU WA KUJIFUNZA.

Ni muhimu sana kujenga tabia ya kujisomea na kufanya maandalizi ya masomo ya siku inayofuata. Nawashauri wazazi kutenga muda wa saa mbili au zaidi kila siku ambazo watoto wao watahitaji kujifunza na kufanya kazi za masomo walizopewa shuleni.

KWA WAZAZI/WALEZI; JIVUNIE SHULE YAKO.

Tafadhali jitahidi kila mara kujivunia shule ambayo mtoto wako anasoma kwa kutaka kufahamu zaidi shughuli zake na kutoa michango ya mawazo wakati ikibidi. Tutafurahi kusikia kutoka kwako kuhusu mawaidha utakayoweza kutupa kuhusu uendeshaji wa shule hii. Timiza wajibu wako kwa mtoto wako na kwa pamoja tutawaendeleza watoto wetu

TANBIHI: Pamoja na maagizo haya tunaambatisha mambo yafuatayo;

(a) Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi ya kukubali nafasi ya masomo shule hii na mzazi kukiri kukubaliana na sheria/kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(b) Fomu ya kupimwa afya.

NIDHAMU:

(a) Wanafunzi wote wanatakiwa kuonesha heshima popote wanapokuwa shuleni na nje ya shule.

(b) Lazima mwanafunzi kuheshimu na kutii viranja na viongozi wengine.

(c) Wanafunzi wanatakiwa kupendana na kuheshimiana wao kwa wao.

(d) Wanafunzi waheshimu na kutii walimu na wafanyakazi wote wa shule.

(e) Ni lazima wanafunzi wawaheshimu viongozi wote wa Taifa na Umma kwa ujumla

(f) Wanafunzi ni lazima wawaheshimu wageni wote wanaokuja shuleni na kuwasaidia inapolazimika

(g) Kuvaa sare ya shule ipasavyo na si vinginevyo – kwa heshima.

<u>MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:</u>

1. Wizi,
2. Uasherati
3. Ulevi wa aina yoyote.
4. Uvutaji wa bangi au sigara.
5. Kuanzisha au kushiriki katika mgomo au fujo hapa shuleni.
6. Kuharibu kwa makusudi na kutokuheshimu bendera ya Taifa, alama ya Taifa, picha ya Rais na Makamu wake.
7. Kuharibu kwa makusudi mali au samani za shule, za walimu au za watu wengine.
8. Kupata mimba na kutoa mimba, kumpa msichana mimba.
9. Kuoa au kuolewa.

Edit with WPS Office

10. Kutohudhuria shuleni mwezi mmoja bila taarifa.
11 Kupigana na Mwalimu, mfanyakazi au mwanafunzi.
12. Kukataa adhabu au hukumu ya Mkuu wa shule .
13. Kudharau au kukataa kushiriki katika shughuli za kujitegemea hapa shuleni.
14. Kupatikana na uhalifu au kujeruhi mtu yeyote katika jumuiya ya shule.
15. Kuja/kuonekana na silaha shuleni/nje ya shule.
16. Kukutwa na simu ya mkononi shuleni.

……

CHARLES T.MKENDA

4

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MJIMPYA
S.L.P 8480,MOSHI-KILIMANJARO

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A.TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI
Jina la mwanafunzi(la mtihani)…….
Tarehe ya kuzaliwa…….
Mahali pa kuzaliwa(wilaya,mkoa)…….
Uraia: Mtanzania/Si Mtanzania…….
Dini……..Dhehebu……

B:TAARIFA YA MZAZI/MLEZI
Jina la mzazi/mlezi…….
Anwani ya mzazi/mlezi…….
Namba ya simu ya mkononi ya mzazi/mlezi……

C:KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO NILIYOPEWA
Mimi ……..kidato cha …… mwaka …….
Ninathibitisha kupokea maagizo na kwamba nimekubali nafasi niliyopewa .
Tarehe……..Saini……

D:KUKUBALI SHERIA ZA SHULE
Mimi……nimezisoma sheria za shule na ninaahidi kwamba nitakuwa mtiifu kwa sheria zote na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu,wafanyakazi wasio walimu na viongozi wote wa shule.
Tarehe……..Saini…….

E.MZAZI/MLEZI

Edit with WPS Office

Mimi ……..(mzazi/mlezi)nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule,yanayohusu mwanafunzi ……..
Ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa kama mzazi/mlezi wa mtoto huyu kwa kushirikim ipasavyo na kumtimizia mahitaji yake ya shule.
Tarehe…….Saini……

NB:
Tafadhali mzazi fika shuleni siku ya jumatatu tarehe 04/01/2021 saa 4:00 asubuhi,ukiwa na fomu hii kwenye kikao cha wazazi ili tujadili kwa pamoja maswala yanayohusu watoto wetu.

THE OFFICE OF PRIME MINISTER REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MJIMPYA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 8480 MOSHI- KILIMANJARO
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

TO THE MEDICAL OFFICER
…….
…….
…….
Please examine ……(name of the student)who has been selected to join this school of his/her fitness as a student in the following areas.
1.Eye Sight……
2.Hearing……
3.Specimen
i.Stool……
Ii.Urine……
Iii.Blood……
4.Asthma……
5.Tuberculosis……
6.Pregnancy……
6.Other Diseases……

Edit with WPS Office

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by medical officer)

I have examined the above and considered that he/she is physically fit/not fit as a student .

Date……Signature……

Station……..Designation……

OFFICIAL STAMP

Edit with WPS Office